

2. Kumwona daktari

Madaktari bingwa

- daktari wako wa familia anawezakutaka umwone daktari bingwa kama unahitaji vipimo au matibabu zaidi. Madaktari bingwa wamesomea utaalumu maalumu wa afya.
- kwa ujumla unapewa barua na daktari wako ili kuonana na daktari bingwa. Unaweza kumwona daktari bingwa bila ya barua ya daktari walakini utapata punguzo la gharama dogo sana kutoka medicare.
- ada ya daktari bingwa kwa kawaida ni kubwa kuliko ada ya daktari wa familia. Wengi wa Madaktari bingwa hawalimbikizi malipo – bulk billing. Ni muhimu kujua ada utakayo tozwa.
- daktari wako wa familia pia anaweza kukuelekeza kwa daktari bingwa katika hospitali ya umma. Itakubidi usubiri kwa muda mrefu ili upate miadi. Madaktari bingwa katika kliniki za wagonjwa wa nje wa hospitali za umma hutoa huduma bure. Vilevile madaktari bingwa hutoa huduma za kibinafsi katika kliniki za hospitali za umma.

Madawa

- daktari wako wa familia na / au daktari bingwa anaweza kukupatia cheti cha madawa. Unapaswa kupeleka cheti hichi kwa duka la dawa au famasia
- unapaswa kuchukua kadi yako ya medicare, kadi ya health care au Kadi ya Pensheni kwa duka la dawa kama unazo. Piga simu Centrelink - lugha mbali mbali 131 202 kuhusu ustahiki wa kadi hizi
- utahitajika kulipia madawa yako lakini mengi ya madawa haya hugarimu bei ya chini kwa watu wenye kadi hizi
- kwa habari zaidi angalia Ukurasa wa maelezo ya 3 - Madawa

Daktari bingwa	Hulenga
Kizio/mtaalamu wa elimu ya kinga maradhi (allergisti/immunilogisti)	mfumo wa kinga (mfano mizio, pumu)
Mtaalamu wa moyo (cardiolojisti)	moyo
Daktari wa ngozi (Dermatolojisti)	ugonjwa wa ngozi
Mtaalamu wa tezi (endocrinolojisti)	Tezi na homoni (mfano - ugonjwa wa kisukari)
Mtaalamu wa uvimbe tumboni (Gastroentolojisti)	Tumbo, maini, mmeng'enywa wa chakula
Daktari wa magonjwa ya wazee	Watu wazee
Gynaekolojisti	Magonjwa ya wanawake
Mtaalamu wa magonjwa ya damu (haematolojisti)	Damu
Mtaalamu wa homa ya manjano (hepatolojisti)	Maini
Daktari wa maradhi ya kuambukiza	Magonjwa ambayo yanaweza kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine mfano tetekuwanga, ukambi, ukimwi
Mtaalamu wa matibabu ya uvimbe (salatani)	Matibabu ya salatani - kansa
Mtaalamu wa uvimbe wa mafigo (Nephrologisti)	Mafigo
Mtaalamu wa nyurolojia (Neurologisti)	Ubongo
Daktari wa uzazi (Obstetrician)	uzalishaji watoto
Wataalamu wa sehemu za kazi	majeraha/magonjwa kazini
Mtaalamu wa macho (ophthalmolojia)	Macho, kuona
Mtaalamu wa tiba ya mifupa (Ophthopaedisti)	mifupa, misuli, viungo
Mtaalamu wa sikio, pua na koo/Daktari wa ENT	sikio, pua na koo
Mtaalamu wa watoto na magonjwa yao	Watoto
Patholojia	Chembechembe na tishu za mwili, kutambua maradhi/ugonjwa
Mtaalamu wa madawa (pharmacolojisti)	Athari ya madawa/madawa katika miili ya watu
Daktari wa Dawa ya Upunguzaji Maumivu	Kupunguza maumivu na kusaidia kuongeza maisha wakati wa ugonjwa na kifo
Magonjwa ya akili (psychiatristi)	ugonjwa wa akili
Mtaalamu wa x-ray (Radiologist)	Kutengeneza na kutafasiri picha za sehemu ya ndani ya mwili (mfano x-ray)
Mtaalamu wa viungo	misuli na mifupa mfano yabisi (arthritis)
Daktari wa upasuaji (Surgeon)	Upasuaji - operesheni
Dawa ya kifua	Kifua, kupumua
Mtaalamu wa mfumo wa mikojo	Eneo la kukojoa, ikijumuisha figo, mji wa mimba, kibofu cha mkojo,